LINDENI ROHO ZENU NA MALI

ZENU-KUZACHA WAMECHACHA

HAPO ZAMANI ilikuwa ni "Congo By Force" waliokuwa wakifanya raia, kuwatesa na kuwanyang'anya mali zao. Wahalifu hawa, walikuwa makao yao ni huko Kongoweya. Baada ya kundi hilo kuanza kutoweka, nako nuko Changamwe kukazuka kundi la uhalifu ambalo lilizua mtindo wa kuwashambulia na kuwaibia raia wasokuwa na hatia kwa kuwashambulia kwa mawe ambayo walikuwa wakiyadai ndani ya pakiti za maziwa. Raia wengi waliopoteza maisha yao na mali yao. Baada ya bidii kubwa ya polisi na raia, wahalifu hawa walianza kutoweka hapa, na ikawa watu wanaweza kutembea tena bila ya hofu ya kuumizwa. Lakini sasa tena pamezuka "Kuzacha".

Kuzacha kwa Kimijikenda ni "kumekucha" ama "kumepambazuka" Kundi hili la wahalifu makao yake makubwa ni sehemu za Majengo. Na kwa mujibu wa mambo tunavyoyaona, kundi hili linapendelea sana kuiba saa za mkono. Wapita njia huibiwa saa za mkono hata saa za mchana. Jamaa hawa hukujongelea kwa hekima na upole, na kabla hujatambua panatendeka nini, huwa saa imekwenda. Iwapo katika kuiba kwao hawakufanyiwa pingamizi, basi kuzacha wanaweza kukuibia bila ya kukujeruhi. Lakini iwapo utajaribu kujitetea, basi hapo ndipo utakapokutana na visanga. Lakini mara nyingi kabla hawajakuibia, huangalia maumbile ya huyo mtu mwenyewe. Iwapo kifua chake kimejaa afya, basi hutumia risasi baridi (zero) kwa kumuagusha kabla ya kumvamia.

Wengi kati ya wanaokumbana na maafa ya Kuzacha ni akinamama na wasichana ambao mara nyingi wao huwa wameyaa mikufu ya dhahabu, bengili pamoja na mapambo mengine. Kwa hivyo siku ya arusi ya Kiswahili huwa si msimu mawindo. Viwindwa huwa ni akinamama walio-jaamba kochokocho kwenda kwenye sherehe za arusi. Lakini iwapo Kuzacha wamekosa vitu vya thamani kama zile mikufu, vidani na saa, basi hata kofia zile zilizo juu pia hufaa kwa kupitisha siku. Kwa hivyo akina baba wamelazimika kulinda mikono pamoja na vichwa vyao wanapotembelea sehemu za Majengo.

Kundi hili la kuzacha ambalo yasemekana kwamba lina vijana wadogo wadogo, lina maskani tafauti hutegemea siku na wakati. Lakini sehemu ya Lohana wakati wa usiku imekuwa ya kutisha sana siku hizi. Lakini jambo la kustajabisha ni kwamba vijana hao ambao wameasisi genge hilo la Kuzacha wote wanajulikana hata kwa majina na baadhi ya watu wanawajua hata maskani yao pia. Ni bwi juzi ambapo Mkuu wa Mkoa wa Mpwani Bw. Luka Galgalo alipoita mwito wa kuwafichua Kuzacha. Sasa jamaa hao wanaowajua Kuzacha mpaka leo wanagojea nini hawawafichui kwa usalama wa wakaazi wa mji wa Mombasa?

Kundi hili la Kuzacha linaendelea na kufanya ukatili kuu kwamba limepawa leseni ya kufanya hivyo. Imekuwa leo katika mji wa Mombasa hakuna uhuru wa kutembea, na ukifanya hivyo utakuwa unahatarisha maisha yako na pia itakubidi utembee kama muhuni yaani uswe na hata kitu kimoja kaitka mwili wako ambacho kingeuzika hata kwa shilingi kumi. Sasa ukitembea katika hali ya utanashati utabiwa na kuzacha na ukitembea katika hali ya uchafu polisi watakubamba kuwa u mzururaji. Je watu sisi tufanyeje hata tuwe katika hali ya usalama?

Hatuwezi kulaumu mtu wala kulaumu Idara ya polisi. Iwapo sisi raia tunawajua wahalifu ni nani, na hatutaki kuwasema kwa wakuu wa usalama ni nini makusudio yetu?

MULUIMA Rober Mdando akipokea zawadi na hati yake baada ya kushinda mashindano ya Plau yaliyofanywa katika kituo cha Diwapa kutoka kwa msaidizi wa Mkuu wa Pwani Bw. Stanley Mutiso Thuku mwenyekiti wa ASK Bw. Kassim Owango na Bi. Mwalle wakitazama. PICHA: NATIONAL STUDIO

KWA DINI YA KIISLAMU MARUNGI NI HARAMU

KULUGU ZANGU Waislamu nawapa nasaha hii, kula marungi kila za kesha au siku yeyote, mujue ya kuwa marungi ni haramu katika Dini ya Kiislamu, walivyo sema Maulamaa wetu limwenguni na madhara yake ni zaidi kuliko tembo. Kwanza ya kwa israfu ya mali, pili inapita wakati wa Swala na wewe una habari, tatu inaharibu akili kama Bangi, kama walivyo thibitisha Ma-Dhaktari katika Hospitali ya Wandazimu.

Nchini na Ulimwenguni Wanawake wengi wameharibika kwa pili ya Marungi na hata hasara sana kwa Wananchi ya

Nchini na Ulimwenguni Wanawake wengi wameharibika kwa pili ya Marungi na hata watoto wadogo wameharibika na afanya wazimu, na utaona Marungi inaliwa sana na Waislamu kuliko wengine wasio kuwa Waislamu.

Naomba Serikali yetu tukufu ichunguze habari hii ya Marungi ambayo inaleta hasara sana kwa Wananchi ya kupoteza sana ku haribu akili, na kuvunja majumba na ku haribu maisha ya watoto kwa ku achana Bibi na Bwana.

Ahmed Bin Yumen MOMBASA.

Waislamu Ujerumani

DINI ya Kiislamu hivi sasa inashikilia nafasi ya pili kati ya madhehebu mbali mbali nchini Ujerumani. Kuna Waislamu wapatao milioni 1.7 Ujerumani ambao milioni 1.4 wakiwa Waturuki, 120,000 kutoka Yugoslavia, 80,000 Waarabu, 20,000 wa asili ya Iran na karibu 1,500 wakiwa Wajerumani wenyewe. Katika Ulaya Uitarama inaongoza kwa kuwa na waumini wengi wa Kiislamu. Ni miji michache sana Ujerumani ambayo haina misikiti ya Kiislamu na si jambo la ajabu kuona waumini wa madhehebu hii wakihudhuria misikitini kila Ijumaa. Hakuna uhaba wa taasisi za madhehebu ya Kiislamu nchini Ujerumani na kwa sasa inakisiwa kwamba Koran Tukufu ni moja wapo ya vitabu vya dini ambavyo vinavyo nunuliwa sana Ujerumani. Pichani panaonekana moja wapo ya misikiti muhimu sana Ujerumani katika mji wa Munich. PICHA: ... RMAN FEATURES

Baadhi ya magadeni ya Mombasa ni makao makuu ya uhalifu, bangi, na miraa

NA ZUBEIR NOOR

NI jambo la kuhuzunisha kuona kwamba zaidi ya Asilimia tisini ya vijana wa jamii ya kiislamu hasa hapa Pwani hupoteza wakati wao mwingi katika Magarden kucheza Draf, Keram Dumna, na kula marungi na kuvuta bangi.

Mbali na hayo mabustani hayo ndipo mahali pa kufanya njama za wizi na uhalifu mwengine ya aina aina. Wengine huwa ndio maskani yao kabisa hula na kulala hapo hapo.

Magarden hayo ambayo yamejengwa bila .mpango wowote ama kuwa na hati yeyote yameweza kujipatia misaada ya pesa taslimu kurekebisha na kuyajenga vizuri ili yawe maridadi. Pamoja na matelevision na vifaa vya michezo niliyotaja imetandazwa na majani na mabaki ya miti ya marungi na huku kukiwa na fukizo maarufu la bangi na vijana wako katika harakati za kucheza keram, drafu na kuangalia TV na kuzugumza lugha chafu.

hapo awali kutoka kwa wanasiasa ambao huwatumia vijana hawa katika kampeini zao za uchunguzi na mambo mengine.

Kitu kengine ambacho nimepeleleza ni kwamba Magarden mengi yapo karibu na Misikiti — ambayo ni nyumba ya Mungu. Mbali na kuwa yanafanya machafu mengi bali inawapinga vijana kumwabudu Mungu kikamilifu. Utakuta katika Magarden kuna video na tape recorders ambazo zina wavutia vijana kuliko kuabudu Mungu.

Ukenda katika magarden haya huwezi kuona japo gazeti wacha Vitabu pekee. Utastaajabu kuona baraza

Ukweli lazima tuseme — ikiwa haya ndio mambo tuyatakayo basi maisha tutakuwa nyuma. Ulisikia hata siku moja garden yeyote ya Mombasa kujitolea kwa damu ama mambo ya kheri? Ikiwa iko garden basi ni kwa ajili ya mwanasiasa fulani basi lakini sio wao wenyewe kuwa na moyo wa kujitolea.

Sidhani wala sifikrii kuwa magarden yanafaa kuwepo au kuwa na manufaa yeyote kwa jamii ila ni ubaya na uharibifu na kuangamiza vijana. Lau **uchukue vijana wote wa magarden alafu upime zile nguvu zao zote za kujenga magarden kama nguvu zile zile tungeweza kujenga majengo yenye manufaa kwa jamii ya waislamu wote. Tungewaomba ndugu hawa wazingatie kwa makini mambo haya kwani "Udongo upatilze ukali maji".**

Tume ya Nidhamu

Pia ingekuwa jambo la maana kwa tume ya nidhamu iliyoundwa hivi majuzi na mtukufu Rais Daniel Arap Moi kuchunguza hatari kubwa inayopatikana kutokana na kuweko kwa magarden katika mitaa. Ikiwezekana yavunjwe ili kuondoa uhalifu na uvutaji wa bangi mitaani.

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD NO 149



KWENDA KULIA:

1. Mbolea
5. Faulu, shinda
7. — — — ya mbali haiui — —
9. Baba mdogo
11. Moja katika nchi za ngambo
13. Ama
15. Kiungo cha maneno
16. Nusu ya neno Dada
17. Jina la kike katika mkoa wa Pwani
18. Mwavumbua, mwabuni
20. Kama No. 9 kwenda kulia
21. Tamko la kukataa.

KWENDA CHINI:

1. Namna ya maradhi
2. Mnyama anayeishi katika ziwa
3. Ikiwa, iwapo kwa Kimomba
4. Hutandikwa nyumbani na lina thamani kubwa
6. Uasi hali ya kutotii
8. Vizia
10. Aina ya mti majani yake hunukia
12. Mmea wenye tunda lenye majina matano
14. Ufuo wa bahari
17. Chombo cha wakati
19. Wakati wa asubuhi.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 148

1. Mrs. Regina Meshack, Sanduku la Posta 90424 Mombasa.
2. Ayubali Jafferbhai, Sanduku la Posta 81666 Mombasa.
3. Hussein A. Sinan, Sanduku la Posta 99247 Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK.*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 148 —

KWENDA KULIA:

1. KANGAROO, 5. RANDA, 6. PAKA, 8. ZAIRE, 11. OA, 12. ZOWEZA, 14. PA, 16. NURU, 17. UZIO, 18. AA.

KWENDA CHINI:

1. KEREZA, 2. GODORO, 3. OLEA, 4. TWAA, 7. KOA, 9. IZARA, 10. EWE, 13. ZIZI, 14. PUA, 15. VOI.

JINA .....

SANDUKU LA POSTA .....

.....

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:-

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-shirt maridadi Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za Fumbo hili lipekelwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270, Mombasa Kenya

Siku ya Jumatano tarehe October 27, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.